TANZANIA STATISTICAL ASSOCIATION

P. O. Box 1174
DODOMA, TANZANIA
Email: tasta.statistician@gmail.com
+255 (0) 754757607/+255 (0) 658750900

# TAARIFA KWA WANACHAMA WOTE WA TASTA KUHUSU MAAZIMIO YA KIKAO CHA KAMATI TENDAJI YA CHAMA

Ndugu Wanachama, kamati tendaji ya chama ilifanya kikao chake cha kawaida kwa mujibu wa Katiba ya chama ibara ya 28(a) tarehe 10/08/2021 na kuongozwa na Mwenyekiti Ndugu Titus Mwisomba. Kikao kilijadili mambo mbalimbali yanayohusu chama. Pamoja na mambo mengine kamati iliazimia mambo yafuatayo;

1. Kuwakumbusha wanachama kulipa ada ya uanachama ya mwaka 2021 pamoja na malimbikizo ikiwa mwanachama anadaiwa ada ya miaka ya nyuma. Kila mwanachama anatakiwa kulipa ada ya uanachama kila mwaka kwa mujibu wa ibara ya 17(a) ya Katiba ya chama.

2. Kwa kuwa siku ya Takwimu Afrika huadhimishwa kila mwaka ifikapo tarehe 18 Novemba, chama kianze maandalizi ya kuhakikisha kinashiriki ipasavyo maadhimisho hayo. Kwa azimio hili, wanachama wote mnaombwa kujiandaa kushiriki maadhimisho haya. Ikiwa mwanachama ana mawazo yoyote juu ya maadhimisho haya na ushiriki wa chama, awasilishe mawazo yake kwa Katibu wa chama. Chama kinaendelea na mipango ya maadhimisho na itakapokuwa tayari wanachama wote watataarifiwa.

3. Kufanya maandalizi ya mkutano mkuu wa wanachama kwa mujibu wa ibara ya 25(a) ya Katiba ya chama. Mipango ya maandalizi ya mkutano mkuu yanaendelea na wanachama wote mtajulishwa tarehe na mahali utakapofanyika mkutano mkuu.

4. Kwa kuwa Katiba ya chama imechapishwa, kila mwanachama ahamasishwe awe na nakala. Nakala ya Katiba inauzwa kwa kila mwanachama kwa shilingi 10,000 (elfu kumi) ili kuongeza mapato ya chama.

Kwa maazimio haya, kamati zote za utekelezaji zinatakiwa kufanya vikao ifikapo tarehe 24/08/2021 na kutoa ushauri ili kufanikisha yale yote yaliyopangwa kutekelezwa.

**KATIBU – TASTA**
**12/08/2021**